**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 03 Mei 2010 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Eleza mambo manne ya kuzingatia wakati wa kufundisha msamiati wa Kiswahili.
2. Taja faida nne za wanafunzi kushiriki katika michezo ya lugha.
3. Toa hoja nne za kuonyesha nafasi ya nyimbo katika malezi ya watoto.
4. Eleza tofauti nne kati ya insha ya simulizi na insha ya maelezo.
5. Toa hoja nne zinazothibitisha umuhimu wa kutumia methali darasani.
6. Eleza mambo manne yanayomwezesha mwalimu kufundisha kwa ufanisi.
7. Taja faida nne za kutumia kazi za vikundi katika ujifunzaji wa Kiswahili.
8. Eleza sifa nne za maandiko bora ya vitabu vya kiada.
9. Toa hoja nne za umuhimu wa Kiswahili katika kuimarisha mshikamano wa Afrika Mashariki.
10. Eleza hatua nne muhimu za mwalimu anapotathmini kazi za wanafunzi.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Jadili nafasi ya vitendawili katika kukuza utamaduni wa Kiswahili.
12. Toa faida tano za kutumia mbinu ya majadiliano katika kufundisha sarufi.
13. Eleza mchango wa kazi za ushairi katika kutunza historia ya jamii.
14. Toa hoja tano zinazoonyesha faida za wanafunzi kusoma magazeti ya Kiswahili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Toa sifa tano za andalio bora la somo.

16. Eleza faida tano za kutathmini wanafunzi mara kwa mara.

17. Jadili mbinu tano zinazomsaidia mwalimu kufundisha kwa ubunifu.

18. Eleza mambo matano yanayoweza kuendeleza stadi za usomaji wa Kiswahili kwa wanafunzi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org